

FOCUS A365

Another Manyamfranchise.Com Evaluation Test

FORM 2 TERM 3 KISWAHILI EXAMINATIONS 2018

MAAGIZO

- (a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- (b) Jibu maswali yote.
- (c) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- (d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- (e) Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
A	20	
B	20	
C	10	
D	10	
E	40	
JUMLA	100	

<http://atikaschool.org>
sales@manyamfranchise.com [0728 450 425]

SOMA USHAIRI UNAOFUATA KISHA UJIBU MASWALI.

Tumeingia uwanjani, kukutana na vijana
Tahiyatuni kaeni, kusikia yenye mana,
Akili zifungueni, mpate kutulizana,
Sigara si ya kuigwa, vijana fikirieni.

Si sinema msidhani, mtaanza kuugua,
Maradhi ya vifuani, mapafu yataungua,
Sijitie ubabeni, kujitia mnajua,
Sigara si ya kuigwa, vijana fikirieni.

Mkingia shughulini, midomo itaungua,
Mtanuka midomoni, thamani kuwapungua,
Mkizitupa makaoni, hasara mtazizua,
Sigara si ya kuigwa, vijana fikirieni,

Ulevi nao acheni, twataka kuwazindua,
Mtangia hatiani, hivyo mnajizuzua,
Wengi hawawathamini, walevi wanapujua,
Ulevi msitamani, vijana fikirieni.

Usingie madawani, kalewa bila kujua,
Si bangi si heroini, siwaze kuzichukua,
Mtangia mashimoni, tubaki tukitundua,
Madawani jitengeni, vijana fikirieni.

Mkijitia uhuni, mjue mtajichubua,
Mpiga ngumi kutani, mazuri hatavumbua,
Ukimwi u mitaani, upesi utawanyakua,
Acheni kuyatamani, vijana fikirieni.

Uvivu nao acheni, utakuja wasumbua,
Vitabu kavishikeni, mazuri mtayavua,
Heshima muithamini, si watu kuwatibua,
Haki zenu zijuchi, vijana fikirieni.

Maswali:

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 2)
- (b) Eleza umbo la shairi hili ukizingatia yafuatayo. (alama 10)
- (i) Mishororo
 - (ii) Vina
 - (iii) Beti
 - (iv) Mizani

(v) Aina ya ushairi

(c) Bainisha matumizi ya uhuru wa mwandishi ukizingatia: . (alama 4)

(i) Inkisari

(ii) Mazda

(iii) Tafsida

(iv) Kufinyanga sarufi/kuboronga

(d) Taja maudhui mawili kutoka shairi hili. (alama 2)

(e) Taja tamathali moja ya lugha na mbinu ya kisanaa (alama 2)

C. ISIMU JAMII

(ALAMA 10)

Taja na ueleze kaida zozote tano za matumizi ya lugha katika jamii.

D. FASIHI SIMULIZI

(ALAMA 10)

Huku ukieleza andika sifa zozote tano za fanani/ mtambaji bora.

E. **SARUFI**

(ALAMA 40)

(a) Taja sifa mbili za kila mojawapo ya sauti hizi /s/ /z/ (alama 2)

(b) Weka shadda kwenye maneno haya (alama 2)

(i) Stima

(ii) Rukwama

(c) Bainisha viambishi katika maneno haya (alama 2)

(i) Walioandikiana

(ii) Vilivyovunjwa

(d) Tumia kihusishi cha mahali kutunga sentensi (alama 2)

(e) Eleza matumizi ya msemu huu (alama 2)
Pua na mdomo'

(f) Eleza dhana ya 'ni' katika sentensi hizi. (alama 2)
(i) Simameni tuombe

(ii) Ninataka tuelewane

(g) Tumia kimilikishi cha nafsi ya tatu umoja kutunga sentensi (alama 2)

(h) Andika maana mbili za sentensi hii: (alama 2)
Mtoto alimlilia mama.

(i) Tumia alama hizi kutungia sentensi. (alama 2)
(i) Mshazari

(ii) Kistari kifupi

(j) Andika sentensi hii bila kutumia 'amba' (alama 2)
Gari ambalo lilinunuliwa jana limeibiwa.

(k) Nyambua vitenzi hivi katika hali ya kutendesha. (alama 2)

(i) Oa

(ii) Kimbia

(l) Kamilisha makundi haya. (alama 2)
Chane ya _____

Shungi la _____

(m) Onyesha matumizi mawili ya kiambishi 'po' katika sentensi moja. (alama 2)

(n) Weka maneno haya katika ngeli mwafaka. (alama 2)

(i) Tikiti

(ii) Dole

(o) Andika sentensi mbili sahihi kwa kurekebisha sentensi hii. (alama 2)
Huku mlimo, panawafaa watu kama nyinyi.

(p) Tumia – zuri kama kielezi, kiwakilishi na kivumishi katika sentensi. (alama 3)

(q) Kamilisha methali hii
Aso hadhari _____

(r) Bainisha aina za maneno
Angelina ni mtoto mtukutu

(alama 2)

(s) Ainisha vitenzi kwenye sentensi hii
Yeye alishindwa kuruka kiunzi kile

(alama 2)

(t) Yakinisha sentensi ifuatayo.
Nisingemuona nisingetimiza ahadi yako

(alama 2)

<http://atikaschool.org>
sales@manyamfranchise.com [0728 450 425]